Kuwa Macho Na Mbwa Mwitu (Watch Out for Wolves)

Na

Ellis P. Forsman

Kuwa Macho Na Mbwa Mwitu

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Kuwa Macho Na Mbwa Mwitu!

Math. 7:15-20

Watu wengi wanapenda kufiria kwamba unaweza kuwaamini viongozi wa kidini.

Wahudumu mara nyingi uhubiri katika mimbari kuhusina na watu unaoweza kuamini.

Watu kila mara wata amini kile ambacho mhubiri, kuhani, au rabi anasema kuwa ni kweli.

Lakini, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa macho na manabii wa uongo.

Math.7:15-20, *"Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua."*

Wanaweza kujitokeza kama kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali,tunatakiwa tuweze kuwatambua, kujua wanachokitafuta. Je leo unawajali manabii wa uongo? Unapaswa kuwa jail!

Mafundisho mengi makuu yanadai kuwa wengi wanaongozwa vibaya. Tunatakiwa tukumbushe hatari, na kujua jinsi ya kuwa weka alama "mbwa mwitu" ye yote ambaye anaweza kuja tulipo!

Kwa maneno ya Mwokozi wetu katika Math. 7:15-20 safi katika akili zetu, napenda kuchukua nafasi hii ili kuweza kujikumbusha "TUwe Macho na Mbwa Mwitu" ebu nirudie kusisitiza pointi kwamba...

Kutakuwa na Manabii wa Uongo

Jinsi Paulo alivyo onya maranyingi...

Kwa wazee wa Efeso. Matendo. 20:28-31, *"Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua na damu yake mwenyewe. Najua mimi yakuwa baada ya kuondoka kwangu, mbwa mwitu wakali wataingia kwenu,*

wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. Kwa hiyo kesheni mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu, usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi."

Ana waambia wajitunze nafsi zao, hata kati yao wenyewe kuna watu ambao wangeinuka, wakiwadanganya watu.

Kwa kanisa la Korintho. 2 Wakor. 11:13-15*, "Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu, maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao."*

Akizungumzia waalimu wa uongo waliokuwepo wakati huo, wakijitokeza kama wahudumu wa kweli, ni kama jinsi shetani alivyojitokeza kama malaika wa mwanga.

Kwa mhubiri mdogo Timotheo.

- 1 Tim. 4:1-3*, "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengi watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe; wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli."*

- 2 Tim. 3:1-9*, "Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasitii wazazi wao, wasio na shkrani, wasio safi, wasio wapenda wa kwao, wasioyaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliyi, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kupenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tama za namna nyingi; wakijifunza siku zote ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli. Na kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, vivto hivyo na hawa wapingana na ile kweli ni watu walioharibika akili zao, wame kataliwa kwa mambo ya imani. Lakini hawataendelea sana; maana upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote, kama vile na upumbavu wa hao ulivyokuwa dhahiri."*

Onyo dhidi ya ukengeufu ambao utakuja, akielezea tabia na mbinu za hao watakao wapotosha watu.

Jinsi waandishi wengine wa Agano Jipya wanavyosema.

Petro, katika kuwaambia kuinuka kwa waalimu wa uongo. 2 Petr. 2:1-3*, "Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia. Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa. Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii."*

Yohana, akiwaita watu "kuzijaribu roho". 1 Yohana 4:1*, "Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetoka kwa Mungu, kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Yuda, akiandika kuhusu baadhi ambao tayari wameshaingia. Yuda 1:3-4*, "Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabithiwa watakatifu mara moja tu. Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tanguzamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliye peke yake Mola, na Bwana Yesu Kristo."*

Kwa maonyo mengine mengi, hili si somo la kuchukua kirahisi! Lakini tutawatambuaje "mbwa mwitu" wanapojitokeza kwa upole (kama kondoo)? Shukrani kwa Yesu na neno la Mungu...

Tunaweza Kuwatambua Manabii wa Uongo

Kwa kuona matunda ya maisha yao.

Tutawafahamu kwa "matunda yao".

Math.7:16-20*, "Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua."*

Kile kilichoko ndani ya mioyo yao itatoka nje, kwa maana katika moyo wa mtu hutoka mawazo mabaya.

Marko 7: 21-23, *"Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivu, uuaji, uzinzi, tama mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi."*

Kwa hiyo, waalimu wa uongo na manabii wa uongo maranyingi wanakanwa...

- Kwa tamaa zao (ilivyo onyeshwa na mtindo wa maisha yao mabovu).
- Kwa ufisadi wao (ilivyo onyeshwa na uhusiano wa uzinzi)
- Kwa kutamani uongozi (jinsi ilivyoonyeshwa na wakuu wa dini).

Nipe muda, matendo ya kweli ya manabii wa uongo itaonekana kwa matunda ya maisha yao!

Kwa kuangalia matunda ya mafundisho yao; kutambua mbinu zao.

Wakifanya kazi kwa siri. 2 Petr. 2:1, *"Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingia kwa werevu uzushi na kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia."*

Badala ya kuwa wazi kwa mmoja na wote. 2 Wakor. 8:20-21, *"Tukijiepusha na neno hili, mtu asije akatulaumu kwa habari ya karama hii tunayoitumikia; tukitangulia kufikiri yaliyo mema, si mbele za Bwana tu, ila na mbele ya wanadamu."*

Wakijieleza kwa tama. 2 Petr. 2:3, *"Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambayo hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii."*

Wanawavuta watu kwa kutumia maneno mazuri ambayo na wao wanapenda kusikia (kama vile afya na utajiri), badala ya kuwaandaa watu kwa kile Wakristo wanaweza kutarajia.

- Matend. 14:23, *"Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini."*
- 2 Tim. 3:12, *"Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa."*

Wakitumia maneno ya udanganyifu.

- 2 Tim. 3:13, *"Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika."*
- 2 Petr. 2:3, *"Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambayo hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii."*

Wakigeuza maandiko ili kuweza kuthibitisha ujumbe wao (ni sawa na jinsi shetani alivyojaribu kumjaribu Yesu), badala ya kushikilia neno la Mungu kwa haki.

2 Tim. 2:14-16, *"Uwakumbushe mambo hayo, ukiwaonya machoni pa Mungu, wasiwe na mashindano ya maneno, ambayo hayana faida, bali huwaharibu wasikiao. Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini, kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu."*

Kutambua mafundisho yao.

Jinsi wanavyo pindua na kuyapotosha maandiko. Wagal. 1:8-9, *"Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri na alaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaniwe."*

Injili yao inaweza kuanza vizuri, lakini wakaibadilisha. Mafundisho yao mara nyingi imewekwa katika kumwelezea mtu, na si maandiko.

Jinsi wanavyofundisha kile ambacho hakika ni kinyume na maandiko.

Kumbu. 13:1-4, *"Kukizuka katikati yako manabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, na tuifuate miungu mingine usiyoijua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii Yule au yule mwotwji wa ndoto, kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, yuawajaribu, apatekujua kwamba mwampenda BWANA Mungu wenu kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata BWANA, Mungu wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye."*

Hata kama wakijitokeza wanakuwa tayari kufanya ishara na maajabu! Jaribio la mwisho ni jinsi wanavyofundisha ukilinganisha na neno la Mungu na lile la mitume wake.

- 1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*
- 1 Yoh. 4:6,*"Sisi twatokana na Mungu. Yeye amjuaye Mungu atusikia; yeye asiyetokana na Mungu hatusikia. Katika hili twamjua Roho wa kweli, na roho ya upotevu,"*

Hitimisho

Haipaswi kuhukumu mioyo ya hao wanaodai kuwa wanazungumza kwa niaba ya Mungu. Tunahitaji tu kuwa "wachunguzi wa matunda". Matunda ya maisha yao na mafundisho yao yatakuwa wazi haraka iwezekanavyo. Hivi ndivyo tunavyoweza "Kuwa Macho na Mbwa Mwitu!"

Hakika, hii inaonyesha kwamba ujuzi wetu kwa neno la Mungu inafaa.....

- Kujua ni nini cha kutafuta katika maisha ya nabii wa uongo.
- Kujua ni nini cha kusikiliza katika mafundisho ya nabii wa uongo.
- La sivyo, hatutakuwa na utofauti na Waisreli, ambao Mungu alisema:

Hosea 4:6, *"Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa: kwa sababu wameikataa marifa, name pia nitawakataa, kwamba hakutakuwa na kuhani kwangu: naona mmesahau sheria ya Mungu wenu, name pia nitawasahau watoto wako."*

Je umeimizwa kuwatambua mbwa mwitu katika mavazi ya kondoo, kama ukimwona mmoja?